

DODOMA

# Sikika yagawa madiwani Kondo

NA KHAMIS MKOTYA

BAADHI ya madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondo, Mkoa wa Dodoma, wamepinga uamuzi wa Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo wa kulifukuza wilayani humo, Shirika lisilokuwa la serikali liitwalo Sikika.

Wakizungumza na MTANZANIA hivi karibuni, madiwani hao walisema uamuzi huo hauna maana kwa kuwa Sikika lilikuwa likisaidia

kuonyesha udhaifu uliopo katika idara ya afya.

Kwa mujibu wa madiwani hao, uamuzi wa shirika hilo kufukuzwa ulianza kutengenezewa mazingira kwa madiwani wa CCM kufungwa na msimamo wa kichama juu ya shirika hilo.

Diwani wa Kata ya Kondo Mjini, Hamza Mafita (CCM), alisema Sikika ni jicho la pili ambalo kama lingetumiwa vizuri na halmashauri hiyo, lingewasaidia madiwani kuona

kasoro za utendaji wilayani humo.

“Kuhusu Sikika, mimi nilijua shirika hili litafukuzwa tu kwa sababu ya viongozi wetu kupenda kulinda ufasadi. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013, miradi ya afya shughuli namba 12 ilitengewa bajeti ya shilingi milioni 17 kwa ajili ya kukarabati vizimba vya kuchomea takataka.

“Ilikuwa ni kwa ajili ya vituo vya afya vya Hamai na Mrijo. Kizimba cha Hamai kilijengwa

chini ya kiwango na thamani yake hata shilingi milioni mbili hazifiki, Mrijo kule hicho kizimba chenyewe hakipo,” alisema.

Diwani wa Viti Maalumu, Hija Suru (CCM), alisema uamuzi wa shirika hilo kufukuzwa ulikuwa na msukumo kwa madiwani.

Hija ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), alisema uamuzi huo haukuzingatia busara kwani

unalenga kuficha maovu na kulinda ufasadi.

“Kabla Sikika haijafukuzwa, madiwani wa CCM tuliitwa katika kikao cha chama, tukaelezwa hoja ya madiwani kutukanwa na Sikika.

“Baadhi tulipinga tukasema hoja ya msingi hapa ni kuhusu ubadhirifu uliojitokeza, tulitaka ripoti ya Sikika ya mwaka 2012 ambayo ilionyesha udhaifu katika miradi ya afya ijadiliwe, ripoti hiyo haikujadiliwa hadi leo,” alisema.